Mei 2016

Mpendwa Muombaji,

Nimekuwa nikiyafikiria maswali kadhaa hivi karibuni: Kwa nini tunaomba? Je, unaomba kwa urahisi tu?

Maombi hayafanyiki kirahisi, na wazo la kuomba kwa sauti linaweza kuleta mashaka kwa baadhi yetu. Hata hivyo, Mungu ni mwaminifu sana anayewaleta wanawake pamoja wakati wa shida na uhitaji kupitia vikundi vyetu vya maombi vya Project Hannah. Vikundi vyetu vya maombi hutupa mahali salama pa waombaji kushirikishana mambo wanayopambana nayo.

Mmoja wa wanawake aliyehudhuria mkutano nchini Afrika Kusini alishukuru Project Hannah kwa kumtia moyo kuja kwenye kikundi cha maombi kila siku ya ijumaa kuomba pamoja na wanawake wengine. Alisema hili lilimsaidia kwenye maeneo mbalimbali ya maisha yake na baadhi ya maombi yake yamejibiwa.

Kikundi kingine cha maombi cha Project Hannah nchini Afrika Kusini kimekuwa kikimuomba Mungu amuwezeshe muamini mpya kwenye kikundi hicho. Mama S anamshukuru Mungu kuwa sasa anaweza kuona. Anashuhuda kuwa alifanywa kipofu na mapepo na alikuwa akiamini miungu. Moyoni alitaka kumtumikia Mungu lakini alikuwa anajaribu kumtumikia Mungu na kuchanganya na miungu yake. Waamini walienda nyumbani kwake na wakamuombea. Mtukuze Mungu kuwa sasa anamtumika Mungu aliye hai tu!

Ninakumbushwa leo kuwa tunapoangalia Biblia tunaona maeneo mengi yanayotuongoza na kukutia moyo kuomba.

- Tunapopata hofu, maombi hutusaidia kupata amani. “Msijisumbue kwa neno lolote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu. Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu.” (Wafilipi 4:6-7). “Nalimtafuta Bwana akanijibi, akaniponya na hofu zangu zote.” (Zaburi 34:4).

- Tunapochoka, maombi hutusaidia kupata pumziko. "Njooni kwangu ninyi nyote mnaosumbuka na wenye kulemewa na mizigo nami nitawapumzisha” (Mathayo 11:28).

- Maombi hutukumbusha kuwa hatupo pekee yetu na kwamba Mungu yupo karibu. “BWANA yu karibu nao waliovunjika moyo, na waliopondeka roho huwaokoa.” (Zaburi 34:18).

- Maombi huyafungua macho yetu kwa mataifa. “Mataifa na washangilie, Naam, waimbe kwa furaha, Maana kwa haki utawahukumu watu, Na kuwaongoza mataifa walioko duniani.” (Zaburi 67:4–5).

Jiunge nasi kuomba mwezi huu kwa ajili ya dada zetu wa Kusini mwa bara la Afrika. “Mbingu na zifurahi, nchi na ishangilie; na waseme katika mataifa, BWANA ametamalaki!’ (1 Mambo ya Nyakati 16:31).

Peggy Banks
Mkurugenzi wa Kimataifa wa Huduma
Project Hannah

**Mtukuze Mungu kwa wanawake jasiri wanaosafiri kwenye nchi za Kusini mwa bara la Afrika kuwaalika wanawake wengine kuomba pamoja nao na kusikiliza vipindi vya Wanawake wa matumaini kwa lugha zao. Omba ili pesa zipatikane kusaidia huduma zinazoanzishwa kwa juhudi kubwa sana ya wanawake hawa.**

Nukuu hizi zimetolewa kwenye taarifa za hivi karibuni kuhusu maeneo yaliyotembelewa ambako Wanawake wanaanzisha huduma mpya za maombi na shughuli zilizoanzishwa na zinaendelea kwenye sehemu hizo.

**Swaziland:**

Mratibu wa nchi wa Swaziland, Khaboe, alisafiri na wanawake 16 kutoka Manzini hadi eneo la Kandinda. Safari hii iliandaliwa na chifu. “Mke wa Chifu alitukaribisha na kufurahia ugeni wetu maana wanaishi kijijini mbali sana na mjini…Tulikuwa na sabuni tulizogawa kwa wanawake; na kila sabuni ilikuwa na andiko la mstari wa Biblia. Walifurahi sana kuzipokea.”

Khaboe aliwashirikisha neno la Mungu baada ya kuitambulisha huduma ya Project Hannah kwa wanawake wa eneo hilo. Walifurahia sana hasa wazo la kuombea wanawake wengine ulimwenguni. Tuliwafundisha habari za Dorcas, mwanamke aliyejitoa kwa vitendo vya ukarimu na kujitoa kuwahudumia watu wa jamii ya Joppa (Matendo ya Mitume 9:36–43). Tunatakiwa kujitolea kuwasaidia wengine na kuwapa wahitaji vitu. Tumewatia moyo wanawake kutenda mambo mema na kuwafikia wenye uhitaji.

**Afrika Kusini:**

Mratibu wa nchi wa Afrika Kusini, Lyn Burnet alisafiri kwa ndege kuwaona wanakikundi cha maombi cha Mkoa wa Kwa Zulu Natal. Kikundi hicho walimueleza Lyn maendeleo ya vipindi vya Wanawake wa matumaini vinavyoandaliwa na redio ya TWR. Pia walitoa taarifa ya shughuli za vikundi vya maombi na wasikilizaji:

- Kikundi cha Umbumbulu kina wanawkae 20 wengi wao ni wajane wanaotamani kumjua na kumtumikia Mungu.
- Kundi la Kwanyswa kikatoa ushuhuda wenye nguvu kuhusu mwanamke mganga aliyempa Bwana maisha yake. Nguvu ya maombi!
- Kundi ambalo liko karibu na bonde la imani nalo linaendelea. Watu wa kwenye kundi hilo wanabadilika. Wanawake wanapata kazi na kuondoka na wapya wanakuja kujiunga.
- Kundi la Molweni wengi wao ni wajane wanaosikiliza vipindi kwa lugha ya kizulu kwenye vifaa vya sauti walivyopewa na kuomba pamoja.
- Nyumba ya maombi ya Umlazi ina vipindi vitatu vya maombi kila siku.

Lyn alipokuwa huko, alipata fursa ya kusafiri na Zoee na Philile kukutana na waombaji wa kikundi cha Umlanzi. Mchungaji Janet amekuwa akikiongoza kikundi hiki tangu 1995. Kwa miaka kadhaa ya karibuni, wamekuwa wakitumia kalenda za maombi za Projech Hannah kwa kuzingatia mahitaji ya maombi hayo. Kwa kawaida walikuwa wanakutana kwenye jumba la mbao lililochoka. Kwa ujio wa Lyn, waliweka hema na walihudhuria wanawake kama 20 kwenye mkutano huo. Walikuwa na muda mzuri wa kushirikishana neno la Mungu na kuomba pamoja. Huwa wanakutana kuomba alfajiri saa kumi na moja, saa nne asubuhi na saa kumi na mbili jioni. Kundi hilo hawana mahali pa kuombea tena kwa sasa maana nyumba ya mbao waliyokuwa wanatumia ilianguka kutokana na mvua. Wanahitaji maombi ili wapate nyumba mpya ya mbao ya kufanyia maombi.

Omba ili waratibu wengi wapatikane kwenye maeneo ya Gauteng, KZN, na Cape Town. Mtukuze Mungu kwa ajili ya Verona, Avrille, Jay, Brenda, Eunice, Linda, Pumla, Ria, Margaret, Geraldine, na viongozi wengine.